

**LALA**

**na**

**Terry Warford**

**LALA**

**na**

**Terry Warford**

**Novemba 6, 2011**

# LALA

Kulala ni sehemu muhimu katika maisha yetu ya kila siku, tukiipa akili zetu mapumziko na miili yetu nafasi ya kupata nguvu. Mungu alitutengeneza ili kupata muda wa kutosha wa kulala kila siku, na zaidi kila wakati, hasa tunapokuwa wagonjwa.

Hata Mungu alikuwa na siku ya kupumzika. Inaongelea umuhimu wa kupumzika unapofikiria vitu vyote vya dhamani amavyo Mungu ameumba kwa siku sita, na hivyo ilikuwa ni siku ya kupumzika akaitakasa. Hebu tusome Mwa. 2:1-3, “*Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibariki siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.*” Kupumzika ni muhimu, na Mungu alifanya usingizi kama njia kuu tunayopata usingizi.

Biblia inasema mengi kuhusu kulala, na kupumzika, na tunapaswa kusikiliza neno la Mungu kuhusiana na somo hili.

Awali ya yote, Biblia inatupatia msaada wa kupata usingizi mnono wakati wa usiku. Hii ilikuwa muhimu kwangu mimi binafsi, kwa sababu nilipitia nilipitia wakati mgumu wa miezi mingi nikikosa usingizi miaka michache iliyopita. Nilikuwa na matatizo ya ki afya, na niliogopa kwa sababu ilikuwa mbaya zaidi ya ilivyokuwa hapo awali. Uoga na hofu ikaifanya kuwa vigumu kupata usingizi, na kukosa usingizi tu ukaifanya mbaya zaidi, ambayo kwa upande mwingine ukaifanya vigumu kupata usingizi. Dawa zilinisaaidia, na nilishukuru kwa hilo. Lakini haikutoa suluhisho la kudumu. Ila wakati wa hali kama hii Bwana akanisaidia kwa maandiko na hakika ikanipa suluhisho na amani ya kudumu

Kimsingi, kile ambacho Biblia kuhusu kupata usingizi mnono ni kumtegemea Mungu, kumwamini katika neno lake, na kwa kile anachosema kufanya kupitia neno lake.

Moja kati ya vitu muhimu inayosababisha kukosa usingizi ni uoga. Kuamini katika Mungu huondoa uoga wa mambo ya kidunia. Kufanya kile ambacho Mungu anasema katika neno lake na kuamini katika ahadi zake inaweza kutuongoza kukaribisha kurudi kwa Kristo, kupumzisha uoga wetu. Na ni kanuni ambayo ipo katika maandiko yote kwamba kama tutafanya mambo kwa njia ya Mungu atatubariki – pamoja, na usingizi mnono wa usiku.

Hebu tuangalie Mit. 3:24, “*Ulalapo hutaona hofu; naam, utalala na usingizi wako utakuwa mtamu.*” Ni nini ambacho kitasababisha usingizi wetu kuwa mtamu? Lazima turudi katika mistari kadhaa ili tupate ni

kwa nini. Tunasoma katika mistari ya 19-24 kwamba ni kwa sababu ya kuamini na kuegemea katika neno la Mungu. *“Kwa hekima BWANA aliiweka misingi ya nchi; kwa akili zake akazifanya mbingu imara; kwa maarifa yake vilindi viligawanyika; na mawingu yadondoza umande. Mwanangu yasiondoke machoni pako, shika hekima kamili na busara. Basi yatakuwa uzima kwa nafsi yako, na neema shingoni mwako, wala mguu wako hautakwaa. Ulalapo hutaona hofu; naam, utalala na usingizi wako utakuwa mtamu.”* Tunapata wapi hekima ya Mungu, uelewa, na hekika, ili kwamba tuweze kuyatunza katika neno lake. Na kutunza vitu hivi katika neno lake inaturuhu kulala kwa amani pasipo uoga. Sasa, tunapoendelea na mistari 25-26 tunapata kwamba tunapomtegemea Mungu inatuwezesha kushinda uoga wa kidunia, alafu pia inatufanya kupata usingizi. *“Usiogope hofu ya ghafla, wala uharibifu wa waovu utakapofika. Kwa kuwa BWANA atakuwa tumaini lako, naye atakulinda mguu wako usinaswe.”*

Angalia katika Walawi 26:3-6, hakika tunaelewa kwamba hii ni sehemu ya sheria ya Musa, na hili si agizo kwetu. Bali mfumo uliohusiswa bado inaweza kutusaidia kulala katika upendo wa kujali wa Mungu. Mfumo tunaoupata ni kwamba tunapoishi maisha yetu kama ambavyo Mungu anaagiza atatubariki kwa njia nyingi, ukijumlisha kulala. *“Kama mkienda katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyafanya; ndipo nitazinyesha mvua zenu nyakati zake, na nchi itazaa maongeo yake, na miti ya mashambani itazaa matunda yake. Tena kupura nafaka kwenu kutaendelea hata wakati wa kuvuna zabibu, na kuvuna zabibu kutaendelea hata wakati wa kupanda mbegu; nanyi mtakula chakula chenu na kushiba, na kuketi na kuketi katika nchi yenu salama. Nami nitawapa amani aktika nchi, tena mtalala wala hapana atakayewatia hofu, nami nitawakomesha wanyama wabaya katika nchi yenu, wala hautapita upanga katika nchi yenu.”*

Hebu tusome Fil. 4:6-7, ambayo inatuambia kwamba Mungu katupatia baraka ya maombi, kutupatia amani ya akili. *“Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia yenu katika Kristo Yesu.”* Hatupaswi kuwa na hofu lini tunapaswa kuomba.

Zab.3:5, *“Nalijilaza nikalala usingizi, nikaamka, kwa kuwa BWANA ananitegemea.”*

Hivyo, kulala ni mufumo wa asili, na neno la Mungu linatupatia muongozo mzuri wa jinsi ya kushinda uoga na hofu ili kwamba tupate usingizi mzuri. Pia inatuambia kwamba tukiishi maisha yetu katika njia ya Mungu atatubariki kwa njia nyingi, pamoja na kulala. Mwongozo tunaoupata ni rahisi – kumuamini Mungu, kuamini katika neno lake, na kufanya kile anacho tuamuru kukifanya.

Kwa upande mwingine, Biblia pia inatuonya kwamba tusijiingize sana katika kulala. Hatutaki kuwa wavivu. Mit. 20:13, “*Usipende usingizi usije ukawa maskini; fumbua macho yako nawe utashiba chakula.*” Mit. 24:30-34, “*Nalipita karibu na shamba la mvivu, na shamba la mizabibu la mtu asiye na akili. Kumbe lote pia limemea miiba; uso wake ulifunikwa kwa viwavi; na ukuta wake wa mawe umebomoka. Ndipo nilipoangalia na kufikiri sana; naliona nikapata mafundisho. Bado kulala kidogo, kusinzia kidogo, bado kukunja mikono upate mikono! Hivyo, umaskini wako huja kama mnyang’anyi, na uhitaji wako kama mtu mwenye silaha.*”

Kimsingi hatupaswi kuwa wavivu, na kulala, kiroho.

Katika 1 Kor. 11:29-30, tunasoma kwamba kama nia zetu hazipo kwa Kristo tunaposhiriki meza ya Bwana, tumelala (kufa) kiroho. “*Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili. Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu waliohawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala.*”

Katika Marko 13:34-37, “*Mfano wake ni kama mtu mwenye kusafiri, ameiacha nyumba yake, amewapa watumwa wake amri, na kila mtu kazi yake, naye amemwamuru bawabu akеше. Kesheni basi, kwamaana hamjui ajapo bwana wa nyumba kwamba ni jioni, au kwamba ni usiku wa manane, au akiwapo jimbi, au asubuhi; asije akawasili ghafla acute mmelala. Na hilo niwaambialo, nawaambia wote, kesheni.*”

Kwa hiyo inaitajika tuamke, na tuwe na shauku na hai katika kazi ya Bwana. Rum. 13:11-12, “*Nm, tukiiujua wakati kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia; kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini. Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru.*”

Kipengele kingine tunayopata kuhusu kulala ni kwamba kifo cha kimwili kinaongelewa kama kulala – kulala kwa muda ambapo tutafufuliwa katika siku hiyo kuu ya hukumu. 1 Wathess. 4:13-18, “*Lakini ndugu hatutaki msijue habari zao waliolala mauti msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tulio salia tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo.*”

Mwisho, sura ya 4 ya Waebrania inazungumzia zawadi yetu ya milele kama kupumzika. Mustari wa 9, *“Basi imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu.”* Mustari wa 11, *“Basi na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.”*

Hivyo, Mungu utubariki na usiku wenye usingizi mnono tunapo mwamini, tukiamini neno lake, na kufanya kile anachotuambia kukifanya. Lakini hatutaki kuzidisha usingizi kiasi kwamba tunakuwa wavivu, hasa katika kazi ya Bwana. Kifo cha kimwili inaongelewa kama usingizi wa muda mfupi ambao tutaamka na kuishi naye milele mbinguni, ambayo pia inazungumziwa kama pumziko.

Ninatarajia kwamba karatasi hii imekuwa ikifundisha. Tutafunga somo letu pamoja sasa. Ni wakati wa kulala.

Usiku mwema,

Ndg. Terry Warford



